

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU

21 MEI, 2021



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA TATU

KIKAO CHA THELATHINI NA TATU – TAREHE 21 MEI, 2021

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Viwanda na Biashara kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA MAMBO YA NJE, ULINZI NA USALAMA:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha

2020/2021 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

272. MHESHIMIWA DKT. RITTA ENESPHER KABATI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itatoa fedha kwa ajili ya ujenzi wa Wodi ya Wanaume, Akina Mama na Watoto katika Hospitali ya Wilaya ya Frelimo katika Manispaa ya Iringa.

273. MHESHIMIWA MWITA KEMBAKI MICHAEL (TARIME MJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni Sheria ipi ambayo ilitumika kuchukua ardhi ya Mlima Nkongore kutoka kwa Wananchi na kulipatia Jeshi la Magereza.

274. MHESHIMIWA ESTHER NICHOLAS MATIKO (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni kwa nini Hospitali ya Mji wa Tarime isipandishwe hadhi na kuwa Hospitali ya Kanda Maalum ya Tarime na Rorya.

275. MHESHIMIWA MICHAEL CONSTANTINO MWAKAMO (KIBAHA VIJIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kutatua migogoro ya mipaka ya Kiutawala baina ya Mikoa, Wilaya na Vijiji hapa nchini.

WIZARA YA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:

276. MHESHIMIWA LATIFA KHAMIS JUAKALI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mpango gani mahsus wa kuwapatia Bima ya Afya Wanafunzi wa Elimu ya Juu na wanaosubiri kupata ajira.

277. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kuwakomboa Wanawake wanaobebeshwa mzigo mkubwa wa kugharamia matunzo ya Watoto bila msaada wa baba.

WIZARA YA FEDHA NA MIPANGO:

278. MHESHIMIWA NICODEMAS HENRY MAGANGA (MBOGWE):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha na Mipango:-


Je, Serikali ina mpango gani wa kufuta madeni ya muda mrefu kwa Wafanyabiashara wa ndani yatokanayo na ukosefu wa elimu juu ya matumizi sahihi ya Mashine za EFD wanayodaiwa na Mamlaka ya Mapato Tanzania.

WIZARA YA KILIMO:

279. MHESHIMIWA MUHARAMI SHABANI MKENGE (BAGAMOYO):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuwaandaa Wakulima wadogo wa Miwa (*outgrowers*) wa Bagamoyo ili kuwa na uzalishaji mkubwa na wenye tija.



WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI:

280. MHESHIMIWA IRENE ALEX NDYAMKAMA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi:-

Je, ni lini Serikali itakarabati Meli ya Mv Liemba pamoja na kujenga Meli mpya ambazo zitachochea ukuaji wa uchumi wa Mkoa wa Rukwa.

WIZARA YA MAJI:

281. MHESHIMIWA KASSIM IDDI IDDI (MSALALA):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itaanza kusambaza Maji kutoka Mradi wa Maji Mhangu – Ilogi katika Kata za Lunguya, Ikinda, Shilela, Sogese na Mega katika Halmashauri ya Msalala.

282. MHESHIMIWA FRANCIS LEONARD MTEGA (MBARALI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji:-

Je, ni lini Serikali itakamilisha ujenzi wa Mradi wa Maji Ruduga – Mawindi ili kuwatua ndoo kichwani Akina Mama wa Mbarali.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA ULINZI NA JESHI LA KUJENGA TAIFA:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupidisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022.

**DODOMA
21 MEI, 2021**

**N. J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**